

Wanafunzi wa Winooski kwa Kupinga Ubaguzi

Mahitaji ya wanafunzi kwa Bodi ya Shule ya WSD

Wanafunzi wa Winooski kwa Kupinga Ubaguzi waliwasilisha madai yao kwa Bodi ya Shule ya WSD Jumatano, Julai 15, 2020. Bodi ya shule walipiga kura kukubali madai yao na watashiriki mpango wa jinsi ya kufanya hivyo katika mkutano wao Jumatano, Julai 22, 2020 .

Hapa kuna mahitaji 8 ya wanafunzi:

1. Kwa mara moja, ku Kuwepo na kampeni kuhusu ukweli juu ya ubaguzi wa rangi. Hii itakuwa kusikiliza wanafunzi, na wazazi wetu kuhusu mambo kama vile upendeleo wa kibaguzi, ubaguzi, na ukosefu wa haki katika Wilaya ya Shule ya Winooski,(WSD) hapo zamani. Tume ao “comminsion”, lazima itoe majibu kwa umma na Bodi lazima ichukue hatua sahihi ili kuhakikisha kuwa matukio kama hayo hayatokei WSD katika siku zijazo.
2. Mwanzoni mwa mwaka wa kitaaluma wa 2020-2021, kuwe na Kamati ya upingaji wa Ubaguzi ambayo wanafunzi wanao pambana na ubaguzi wa rangi, upendeleo na ubaguzi wengine wowote, wanaweza kuripoti moja kwa moja matukio hayo.
3. Badilisha Afisa Rasilimali wa Shule (SRO) na wataalam wawili (2) wenye wana elewa hali yakuwa na shida za kiwewe ao “trauma” ili kufanya kazi na wanafunzi kutoka sule la msingi hadi la secondari.
4. Mwisho wa Msimu wa 2020, toa hadharani mpango wa kuajiri walimu wa rangi hapa shuleni mwa winooski- WSD. Lazima pia iweze kuji tokelezea kwa uwazi kuhakikisha kuwa angalau 15% ya wafanyikazi wote na walimu wa WSD ni waalimu wa rangi kwa mwaka wa masomo 2022-2023.
5. Mara moja toa ombi kwa walimu wote kuigiza sehemu za mtaala wa masomo ya kikabila na ufundishaji wa ubaguzi wa rangi ndani ya mtaala wa shule ya winoski kutoka shule ya msingi hadi la secondari (K-12). Lazima pia kuepo na mpango wa masomo wa kikabila unaofadhiliwa kabisa kwa mwanzo wa mwaka wa masomo 2022-2023.
6. Fanya kamati ya ma rudilio ifikapo mwisho wa Agosti 2020 ili iwe na jukumu la ku angalia na ku kagua mtaala uliopo, mazoea ya ufundishaji, na muundo wa sera ili kuhakikisha kwamba wanakubali masomo ya kikabila ya kisasa na viwango vya kupinga ubaguzi wa rangi, matarajio, na mazoea ya kufundisha.

7. Ajiri mtaalamu juu ya haki za raia za kukaribisha semina za mara mbili kwa mwaka ambazo hutakuwa na fundisha na kuunga mkono wazazi na wanafunzi katika kuelewa jinsi ya kutetea watoto wao na haki zao za elimu huko WSD. Fursa hizi lazima zizingatie kanuni za shirikisho na za mitaa zinazohusiana na haki za wanafunzi wa "ELL" yaani wanafunzi ambapo kingereza sio lugha yao ya kwanza, pamoja na wanafunzi wenye ulemavu, haki za raia na sheria za kupinga ubaguzi, na majukumu ya shule kwenye maeneo kama ushiriki wa familia na kusaidia wanafunzi wa kipato cha chini. .

8. Mwanzoni mwa mwaka wa masomo 2020-2021, anzisha mpango wa uhamasishaji kwa wanafunzi ambao kingereza sio lugha yao ya kwanza (ELL), Yaani kuwe na wa sahidizi kwa wanafunzi wa ELL, ili wa endelee na ushauri wa jamii kwa lengo la kuboresha ujuzi wao wa lugha ya Kiingereza na kupata mshirika wa utetezi katika jamii.